JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS-TAMISEMI

HALMASHAURI YA MJI WA KASULU

Namba za simu:
Mkuu wa shule :0759-868-746
Makamu Mkuu wa shule:0767-898-247
27/05/2021
Email :kigomagrand@gmail.com

Shule ya Sekondari Kigoma Grand,

Kasulu.

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi…….
……
S.L.P……
Email:……..

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KIGOMA GRAND KIDATO CHA TANO 2022 HALMASHAURI YA MJI KASULU- KIGOMA

1. Nafurahi kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka 2022 ,tahasuzi ya PCM/PCB/CBG. Shule ya sekondari kigoma grand ipo Mkoa wa Kigoma Wilaya ya Kasulu, Halmashauri ya Mji Kaulu. Shule ipo umbali wa kilometa tano (05)toka kituo cha mabasi yatokayo na yaendayo mikoani kuelekea Kibondo eneo la Mubondo,kama unatoka Mikoa ya Shinyanga,Mwanza,Geita,Bukoba,Mara, na Simiyu waeleze madereva kuwa kituo chako ni Mubondo kwani utakuwa umefika moja kwa moja hapa shuleni. Mikoa mingine ni lazima ufike kituo cha mabasi na utafute usafiri wa kukuleta shuleni Kigoma grand eneo la Mubondo.

   Muhula wa masomo unaanza tarehe 01/06/2022 hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti hapa shuleni tarehe 01/06/2022

2. **MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIWA**.

   2.1 . **SARE ZA SHULE DARASANI (WAVULANA)**

   (a) Sare ya shule hii ni suruali mbili (02) dark blue
   (b) Shati mbili (02) nyeupe za mikono mirefu zisizo na mchanganyiko na rangi nyingine.
   (c) Tai dark blue ndefu za kawaida mbili (02)
   (d) Viatu jozi mbili (02) rangi nyeusi (visiwe na visigino vilefu au buti) na viwe na kamba
   (e) Soksi nyeusi zisizo na mchanganyiko wa rangi nyingine
   (f) Sweta rangi ya kijivu
   (g) Mkanda wa kuvalia suruali ni nyeusi wa ngozi na siyo wa tambi au inta.

   2.2 SARE ZA BWENI -WAVULANA (SHAMBA DRESS)

   (a) Suruali mbili (02) rangi ya kaki mpauko yenye linda mbili kila upande wa furu up.
   (b) T-shirt itapatikana hapa shuleni kwa Tsh. 15,000/=

(c) Nguo za michezo (track suit, bukta, raba, vyote viwe ni dark blue)
(d) Njoo na gumboot

2.3 SARE ZA SHULE ZA DARASANI (WASICHANA)

(a) Sare ya shule hii ni sketi mbili (02) dark blue, zenye linda box kubwa ndefu kupita magoti.
(b) Shati mbili (02) nyeupe mikono mirefu.
(c) Soksi nyeupe ndefu jozi mbili (02)
(d) Raba kwa ajili ya michezo
(e) Viatu vyeusi vya ngozi vya kamba visivyo na kisigino kilefu (yeboyebo hazitakiwi) kiwi nyeusi na brash ya viatu.
(f) Sweta rangi ya kijivu.
(g) Vazi la hijabu linatakiwa kuwa lenye kitambaa kizito cheupe kisichoonyesha maumbile na liwe refu.

2.4 SARE ZA BWENI -WASICHANA (SHAMBA DRESS)

(a) Sketi mbili (02) rangi ya kaki mpauko yenye linda kubwa ndefu kupita magoti.
(b) Nguo za michezo (track suit, raba vyote view ni dark blue)
(c) Njoo na gumboot.

3. **ADA NA MICHANGO YA SHULE**.

3.1 Ada ya shule ni tshs. 70,000/= kwa kila mwanafunzi wa bwenini.unaweza kulipa kiasi cha Tshs.35,000/= kwa kila muhula au kulipa zote kwa pamoja.

3.2 Michango inayotakiwa kulipwa kwa kila Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi:-

3.2.1 Shiling 6,000/= kitambulisho.
3.2.2 Shilling 20,000/= taaluma
3.2.3 Shilling 30,000/= wapishi,walinzi, na vibarua wengine wa shule
3.2.4 Shilling 2,000/= Nembo ya shule.
3.2.5 Shilling 10,000/= huduma ya kwanza.
3.2.6 Shilling 20,000/=Mitihani ya kujipima (mock)
3.2.7 Shilling 5,000/= tahadhari (haitarejeshwa)
3.2.8 Shilling 15,000/= ukarabati wa samani.

Angalizo :*Jumla ya michango na Ada ni Tshs. 178,000/=.****fedha hizo zilipwe kwenye Akaunti ya shule*** A/C **Na. *51410019372*** *jina la Akaunti***KIGOMA GRAND SECONDARY SCHOOL CAPITATIONS FUND (NMB)**(Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip sawa na jina analotumia)
"HAUTA POKELEWA ENDAPO HUTA KAMILISHA YOTE YANAYOTAKIWA SHULENI"

4. Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-

4.1 Njoo na ream moja ya karatasi (A4) kwa mwaka
4.2 Godoro la sponji ($2^1/_2$ ft)
4.3 Shuka mbili rangi ya light blue,blanket,mto, taulo na chandarua.
4.4 Ndoo mbili (02) zenye mifuniko (lipo tatizo la maji bila ndoo utapata shida)
4.5 Daftari kubwa (quire three,four)10
4.6 Dissecting kit kwa wanafunzi wa Biologia
4.7 Scientific calculator
4.8 Vyombo vya chakula (kijiko,sahani,bakuli na vikombe) visiwe vya plastic
4.9 Kwanja (01), jembe (01) mopa (01) mfagio wa mti na hard bloom.
4.10 Njoo na koti la maabara (laboraoty coat) lenye rangi nyeupe mikono mirefu kupita magoti.
4.11 Njoo na passport size tatu za rangi (ipigwe akiwa amevaa shati jeupe)
4.12 Njoo na sanduku la chuma au bati lisiwe begi na uwe na kufuli mbili (02)
4.13 Njoo na tochi/taa ndogo moja duara ya betri (itatumika iwapo umeme umekatika).

4.14 Njoo na vifaa vya usafi binafsi kama vile mswaki,dawa ya meno,mafuta, sabuni za kufulia na kuogea pamoja na kandambili za kuogea aina ya bata.

4.15 Njoo na kifaa cha kuhifadhia maji safi ya kunywa (dumu lita 5)

4.16 Uje na vitabu vya masomo husika kulingana na tahasusi yako ulivyochaguliwa kama.

Pure mathematic 1&2, basic Applied Mathematics, Human and economic Geography,general geography in diagram,Advice inorganic chemistry,organic chemistry,conceptual chemistry, Advice level physics 7th Edition ,Biuological science 3th Edition.

***NB*:**Ni muhimu ununue vitabu vyako mwenyewe kwa sababu shule haina vitabu vya kutosha kwa kila mwanafunzi. Ombi langu kwa wazazi/walezi kughalimia elimu ya mtoto wako kwa ubora wa elimu yake.

5. MATIBABU

Shule itatoa huduma ya kwanza tu, Mwanafunzi atakayeugua atagharimia matibabu ya ugonjwa wake mpaka atakapopona. Shule itafanya utaratibu wa kutafuta bima ya Afya CHF kikaya kwa kupitia malipo atakayolipia mwanafunzi.

6. LIKIZO

Mihura ya shule ni kama ifuatavyo:-

Muhula :**I** utaanza tarehe 01/06/2022 na kumaliza tarehe **03/12/2022** Wanafunzi hawa hawaruhusiwi kubaki shuleni wakati wa likizo.

7. NGUO ZA NYUMBANI

Mwanafunzi wakati wote awapo shuleni atapaswa kuvaa sare za shule tulizo agiza katika barua hii na sare ya bwenini.Hivyo asije na nguo za nyumbani kwa sababu hazitopata muda wa kuvaliwa. Akikutwa na nguo za nyumbani katika sanduku au begi zitachukuliwa na hazitarudishwa na kupewa adhabu nyinginezo dhidi yake itatolewa.

8. SIMU SHULENI HAZIRUHUSIWI.

Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki simu.Akipatikana na simu shuleni atanyanganywa na kuharibiwa na atafukuzwa shule ."Ni vema asije na simu kabisa" upo utaratibu umeandaliwa kwa mwanafunzi kutumia simu ya shule kulingana na uzito wa shida ya mwanafunzi.

9. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na 25 ya mwaka1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:-

(a) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
(b) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
(c) Kutunza mali ya umma.(viti,meza ,vitanda na vioo vilivyo wekwa kwenye madarasa, bweni na bwalo la chakula) uharibifu wowote utaghalimu fedha kwa mzazi kulipa.
(d) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
(e) Kuwahi katika kila shughuri za shule na nyingine utakazo pewa kufanya.
(f) Heshima kwa viongozi,wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
(g) Kuzijua sheria za shule na kuzitii bila shuruti (kama vile kanuni za bwenini, darasani, na bwaloni)
(h) Pesa ya mwafunzi (pocket money) zitatunzwa ofisi ya mkuu wa shule.Mwanafunzi haruhusiwi kutunza bwenini kiasi kinachozidi shilingi 5,000/=.

10. MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE.

i. Wizi (wa aina yoyote ile)
ii. Uasherati,ushoga na ubakaji
iii. Ulevi wa pombe au madawa ya kulevya (bangi,mirungi,kubeli,cocaine n.k)
iv. Kupigana au kupiga
v. Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma.
vi. Kudharau Bendera ya Taifa

vii. Kuoa au kuolewa
viii. Kumpa mimba mwanafunzi
ix. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
x. Kukataa adhabu kwa makusudi
xi. Mwanafuzi kuwa na simu shuleni.
xii. Kuwa nje ya mipaka tya shule bila kuwa na ruhusa ya mwalimu
xiii. Kutuhudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
xiv. Kutoa lugha chafu kwa wanafuzi wenzake,kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule
xv. Kufuga ndevu
xvi. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
xvii. Kudharau Bendela ya Taifa
xviii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu na uharibifu wowote ule wa mali ya umma kwa makusudi.

Endapo mwanafunzi atavunja kanuni/Sheria za Shule, atapewa adhabu moja wapo au zaidi ya zifuatazo:-

(a) Kuchapwa viboko visivyo zidi vinne kwa kila kosa
(b) Kufanya kazi ngumu
(c) Kupewa onyo la maandishi
(d) Kusimamishwa shule
(e) Kufukuzwa shule.

11. VIAMBATANISHO NA FOMU MUHIMU

(a) Fomu ya uchunguzi wa Afya (medical examination) ambayo itajazwa na mgaga wa hospital ya serikali.
(b) Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi.
(c) Picha nne za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea shuleni pamoja na namba zao za simu.

12. AHADI KWA SHULE

AHADI NA UTII WA SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE NIWAPO SHULENI

Mimi ……naahidi kwamba nitafuata na kutii kwa muda wote nitakao kuwa ninasoma hapa shuleni, kanuni na sheria zilizowekwa na Shule.

Sahihi …… Tarehe ……

Tanbihi ;Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyafanyia kazi kikamilifu.

Namba ya simu ya mzazi au mlezi……

KARIBUNI SANA SHULE YA SEKONDARI KIGOMA GRAND
"KIGOMA GRAND HIGH SCHOOL"

SEVERINO M. MANYOTA
MKUU WA SHULE



SHULE YA SEKONDARI KIGOMA GRAND

AHADI YA MWANAFUNZI KUKUBALI KUTII SHERIA ZA SHULE.

Mimi …….. ……

Naahidi kwamba nitafuata na kutii kwa muda wote nitakaokuwa ninasoma Shule ya Sekondari KIGOMA GRAND,kanuni na sheria zote zifuatazo za Shule hii.

NI MARUFUKU:

1. Kuanzisha/ kushiriki kwenye migomo, fujo au ukaidi wa aina yoyote, daima nitatumia taratibu halali ili kutafuta ufumbuzi wa matatizo yaliyojitokeza.
2. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma, picha za viongozi wa Serikali na Bendera ya Taifa.
3. Kuiba
4. Kuwa mwasherati
5. Kutumia kileo na pombe ya aina yoyote
6. Kuvuta sigara au bangi
7. Kupatikana na makosa ya jinai
8. Kupata au kutoa mimba au kumpa mimba mwanafunzi au raia wa nje ya Shule.
9. Kupigana
10. Kutoroka au kutohudhuria shuleni bila taarifa maalum
11. Kwenda nje ya Shule bila Sare au Ruksa ya Mwalimu wa Zamu.
12. Kuoa au kuolewa
13. Kuwa katika kumbi za starehe kama Disco, baa n.k
14. Kumiliki simu nikiwa Shuleni

Endapo nitavunja Sheria mojawapo kati ya hizo nitakuwa tayari kupokea adhabu mojawapo au zaidi kati ya zifuatazo:-

(a) Kuchapwa viboko (visivyozidi vinne kwa kila kosa)
   (i) Matakoni (Wavulana) kwa kulala chini
   (ii) Mikononi (Wasichana)

(b) Kufanya kazi ngumu kama vile, kutengeneza barabara, kuchimba shimo la takataka, kufyeka nyasi/ vichaka, kuokota mawe, kung'oa visiki n.k
(c) Kupewa onyo kali kimaandishi
(d) Kusimashwa shule kwa muda.
(e) Kufukuzwa shule.

MWISHO: gharama zote za kwenda nyumbani na kurudi Shuleni ni juu ya Mzazi/ Mlezi wako.

……. …….

Sahihi ya Mwanafunzi Jina na sahihi ya Mzazi/Mlezi

Tarehe: …… Tarehe: ……

SHULE YA SEKONDARI KIGOMA GRAND

HISTORIA YA MWANAFUNZI

1. Jina la mwanafunzi ..... Dini /Dhehebu .....
2. Jina kamili la Baba .....
3. Je Baba yuko hai au amefariki .....
4. Kama amefariki taja tarehe au mwaka aliofariki .....
5. Jina kamili la Mama .....
6. Je mama yuko hai au amefariki .....
7. Kama amefariki taja tarehe au mwaka aliofariki .....
8. Anuani ya Mzazi .....
   S.L.P .....

9. Kazi aifanyayo Baba .....
10. Sehemu anayofanyia kazi .....
11. Kazi aifanyayo Mama .....
12. Sehemu anakofanyia kazi .....
13. Kama huishi na Mzazi wako taja jina la Mlezi wako .....
14. Kazi aifanyayo.....
15. Sehemu anakofanyia kazi .....
16. Anuani ya Mlezi .....

S.L.P .....

17. Habari nyingine za familia ;

Jina la Kaka / Dada	Umri	kazi yake	Mahali anapofanyia kazi Kama ni mwanafinzi taja Shule.
(a)	.....	.....	.....
(b)	.....	.....	.....

18. Afya ya Mwanafunzi (Tafadhali eleza kama una ugonjwa wowote ambao una kukabili kwa hiyo unastahili huduma muhimu) Ni muhimu umfahamishe Daktari atakaye kupima ili naye aweze kujaza katika sehemu inayomuhusu kwenye fomu kwa ushauri zaidi wa kitaalamu.
    .....
    .....
19. Uthibitisho wa Mwanafunzi;
    Nathibitisha kuwa maelezo niliyoandika katika fomu hii ni sahihi.
    Sahihi .....
    Tarehe .....

AFFIDAVITY FORM

(To be filled by Tanzanians only)

I ..... Tanzania, do here make out and state I am the father/ mother /relative of .....

was born at .....

on the .....day of .....19 .....

And that I was present at/shortly after the birth of the said .....That

had personal and direct knowledge of the said .....on account of

.....

.....

.....

(Describe the circumstances of such personal and direct knowledge) of said ..... Was a Girl/Boy.

Signed .....
Sworn at ..... This day .....
Day of ..... 201 .....
Before me .....
Qualification .....
Address .....
Signature .....

(Official stamp or seal)

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE AND TECHNOLOGY

KIGOMA GRAND SECONDARY SCHOOL.

FORM FOR MEDICAL EXAMINATION.

(To be completed by a Medical officer in respect of all form Entrance)
Pupil's full name ……
Age …… (**Year**) …… Sex ……
Stool examination ……
Urinalysis ……
Blood count (**Red and White**) ……
Syphilis Test ……
T.B Test ……
Eye Test ……
Additional information eg. Physical defect or impairment(**s**),chronic infections or family diseases
……
……
……
……
I certify that I have examined the above pupil and recommend that he/she is fit/ unfit to pursue further education
Signed ……
Designation ……
Official Stamp:

Date: ……
(Delete whichever is in applicable)